

Bodi za Maji za Mabonde

Bonde ni nini?



Bonde la Ziwa Rukwa

Hili ni eneo lote ambalo mwelekeo wa maji yake hatimaye huingia katika Ziwa Rukwa. Eneo hili linajumuisha mikoa ya Mbeya, Rukwa, Katavi na sehemu ndogo ya mkoa wa Tabora.

Bonde la Ziwa Nyasa

Hili ni eneo lote ambalo mwelekeo wa maji yake hatimaye huingia katika Ziwa Nyasa. Eneo hili linajumuisha mikoa ya Mbeya, Njombe na Ruvuma.

Bodi hizi zinasimamia na kuratibu matumizi ya maji katika mabonde..



Bodi ya Bonde la Ziwa Rukwa
P.O. Box 762, MBEYA
+255 2500028
rukwabasin@yahoo.com
www.lakerukwabasin.co.tz



Bodi ya Bonde la Ziwa Nyasa
P.O. Box 240, TUKUYU
0754 769622 / 0753398141
nyasabasin@yahoo.com
www.lakenyasabasin.com

Vibali vya matumizi ya maji


Fuata Taratibu za kisheria kupata kibali



Wizara ya Maji

Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Rukwa
Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Nyasa





Changamoto

zilizopo kwenye Rasilimali Maji

Maji ni muhimu kiuchumi, kijamii na kimazingira. Matumizi ya maji yanapozidi uwezo wa vyanzo husababisha upungufu na kupeleka ukosefu wa maji.

Migororo imeongezeka katika jamii kati ya watumiaji maji mbalimbali kama kilimo na ufugaji nk


Kuongezeka kwa magonjwa yanayosababishwa au kuenezwa na ukosefu au uhaba wa maji.

Kimsingi usimamizi na ugawaji wa maji huhitajika. Tunatambua kuwa Maji yote ni mali ya Taifa na yana-simamiwa chini ya sheria ya usimamizi wa rasilimali za maji Na. 11 ya mwaka 2009.

Faida

ya kuwa na kibali

- Kuwa na haki ya kulindwa kisheria.
- Kuepuka migogoro au migongano ya matumizi ya maji.
- Kuwa na haki ya kukopesheka katika taasisi za kibenki kwa kutumia kibali chako.
- Kuwa na haki ya kupata ufadhili kwa wahisani mbalimbali.
- Kujihakikishia matumizi bora ya maji katika chanzo chako.



TARATIBU

za kupata kibali cha kutumia maji

- 1 Mwombaji wa kibali ataandika barua ya maombi kwa Afisa wa maji.
- 2 Kulingana na aina ya matumizi ya maji Mwombaji atapata fomu ya maombi kwa kulipia
- 3 Afisa wa maji atawasiliana na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi mtendaji wa wilaya ili kupata maoni juu ya chanzo cha maji. Afisa wa maji wa Bonde atatangaza maombi hayo kwenye gazeti la serikali.
- 4 Afisa maji atapima chanzo cha maji husika ili kujua kiasi cha maji kilichopo.
- 5 Mwombaji atawasilisha fomu ya tathmini ya athari za mazingira (EIA) ikiwa mraadi utakuwa na athari za mazingira
- 6 Afisa wa maji wa Bonde atawasilisha barua za maombi kwenye Bodi ya maji ya Bonde.
- 7 Bodi ya maji ya bonde inaweza kutoa kibali cha matumizi ya maji kama mwombaji atatimiza vigezo .